JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

*Dar es Salaam, 03 Septemba, 2025*

# TAARIFA KWA UMMA

## KUKAMILIKA KWA AWAMU YA KWANZA NA KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA PILI YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KWA MWAKA WA MASOMO 2025/2026

### 1.0 KUKAMILIKA KWA AWAMU YA KWANZA YA UDAHILI 2025/2026

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inaufahamisha umma, Taasisi za Elimu ya Juu na wadau wa Elimu ya Juu ndani na nje ya nchi kuwa Awamu ya Kwanza ya udahili wa Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2025/2026 imekamilika. Majina ya waliodahiliwa katika awamu hii yanatangazwa na vyuo husika.

Katika Awamu ya Kwanza ya udahili, jumla ya waombaji **146,879** wametuma maombi ya kujiunga katika vyuo **88** vilivyoidhinishwa kudahili wanafunzi katika Shahada ya Kwanza. Aidha, jumla ya programu **894** zimeruhusiwa kudahili ikilinganishwa na programu **856** mwaka 2024/2025, ikiwa ni ongezeko la programu **38** za masomo. Vilevile kwa upande wa nafasi za udahili, mwaka huu kuna jumla ya nafasi **205,652** ikilinganishwa na nafasi **198,986** mwaka uliopita. Hili ni ongezeko la nafasi **6,666** sawa na asilimia **3.3** katika programu za Shahada ya Kwanza.

Pia katika Awamu ya Kwanza ya udahili, jumla ya waombaji **116,596** sawa na asilimia **79.4** ya waombaji wote walioomba udahili, wamepata udahili kwenye vyuo walivyoomba. Idadi ya waombaji wa udahili na watakaodahiliwa inatarajia kuongezeka katika Awamu ya Pili ya udahili.

### 2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA

Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja wanapaswa **kuthibitisha** udahili wao katika chuo kimojawapo **kuanzia leo tarehe 03 hadi 21 Septemba, 2025**. Uthibitisho huo unafanyika kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya



Jengo la SUMA JKT, S.L.P 2600, 1 Mtaa wa JKT, 4110 Tambukareli, Dodoma
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz

vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika.

Aidha, uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili. Kwa urahisi wa rejea, orodha ya majina ya waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja inapatikana ~~kwenye~~ tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

## 3.0 KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA PILI YA UDAHILI 2025/2026

**Tume inatangaza kuwa Awamu ya Pili ya udahili wa Shahada ya Kwanza kwa mwaka wa masomo 2025/2026 imeanza leo tarehe 03 hadi 21 Septemba, 2025.** Tume inawaasa waombaji ambao hawakuweza kutuma maombi ya udahili au hawakuweza kupata nafasi ya kudahiliwa katika Awamu ya Kwanza kutokana na sababu mbalimbali, watumie fursa hii vizuri kwa kutuma maombi yao ya udahili kwenye vyuo wanavyovipenda.

Aidha, Tume inaelekeza Vyuo vya Elimu ya Juu nchini kutangaza programu ambazo bado zina nafasi. Waombaji udahili na vyuo wanapaswa kuzingatia utaratibu wa udahili wa Awamu ya Pili kama ilivyooneshwa kwenye kalenda ya udahili iliyoko katika tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

## 4.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika. Kwa wale ambao watapata changamoto katika kujithibitisha, vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao na kutafuta ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa.

Imetolewa na:

Prof. Charles D. Kihampa
**KATIBU MTENDAJI**
**TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA**



Jengo la SUMA JKT, S.L.P 2600, 1 Mtaa wa JKT, 4110 Tambukareli, Dodoma
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, S.L.P 6562, 7 Mtaa wa Magogoni, 11479 Dar es Salaam,
Simu: +255 22 2113694, 2113691, Nukushi: +255 2113692, Barua Pepe: es@tcu.go.tz, Tovuti: www.tcu.go.tz